KOM SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 899 – SHINYANGA
Tel: 028-2763596 **Cell:** 0767-483046, 0766-893165 **FAX**: 028-2763564
E-mail: komsecondary@komclass.com

ADA, USAJILI, SARE NA MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI - 2016

1. ADA:

Na.	MAELEZO	MUHULA WA KWANZA GHARAMA (TSHS)	MUHULA WA PILI GHARAMA (TSHS)
1	Ada ya masomo (tuition fees)	450,000/=	450,000/=
2	Ada ya bweni (boarding fees)	600,000/=	600,000/=
JUMLA KWA MUHULA		**1,050,000/=**	**1,050,000/=**
			JUMLA KWA MWAKA **2,100,000/=**

Jumla ya ada ya masomo na bweni kwa mwaka ni **Tshs. 2,100,000/= (**Ada ya masomo **Tshs. 900,000/=** na gharama ya bweni ni **Tshs. 1,200,000/=)**. Jedwali hilo hapo juu linaonesha mchanganuo wa malipo. Malipo yanaweza kufanywa kwa ***Mkupuo Mmoja*** **TShs. 2,100,000/=** au kwa ***Muhula Mmoja*** **TShs. 1,050,000/=** au kwa ***Nusu Muhula*** (Robo mwaka) **TShs. 525,000/=**

2. MALIPO MENGINE (USAJILI, TAHADHARI NA KITAMBULISHO):

Utatakiwa kulipa kiasi cha **TShs. 105,000/=** kwa ajili ya Usajili, kitambulisho na tahadhari mara tu baada ya mtoto kuchaguliwa. (Usajili **TShs. 50,000/=** tahadhari **TShs. 50,000/=** na kitambulisho **TShs. 5,000/=**)

3. SARE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE:

i. **SARE ZINAZOPATIKANA SHULENI**

Ili kuwepo na mfanano wa sare za shule na kudhibiti nidhamu, sare na mahitaji mengine yaliyo orodheshwa katika jedwali hili hapa chini zinapatikana shuleni. Utatakiwa kulipa pesa benki na kisha kuleta bank ***pay-in slip*** shuleni. Mwanafunzi atapewa sare na vifaa hivi siku ya kufungua shule.

WAVULANA			WASICHANA		
SARE	**IDADI**	**GHARAMA**	**SARE**	**IDADI**	**GHARAMA**
T- Shirt	2	25,000/=	T- Shirt	2	25,000/=
Sweta	1	25,000/=	Sweta	1	25,000/=
Shati	2	25,000/=	Shati	2	25,000/=
Suruali - kijivu	2	35,000/=	Sketi - kijivu	2	35,000/=
Suruali - nyeusi	2	35,000/=	Sketi - nyeusi	2	35,000/=
Tai	1	6,000/=	Tai	1	6,000/=
Soksi	2	7,000/=	Soksi	2	7,000/=
Shuka	3	39,000/=	Shuka	3	39,000/=
Godoro	1	55,000/=	Godoro	1	55,000/=
Neti	1	13,000/=	Neti	1	13,000/=
JUMLA		**265,000/=**	**JUMLA**		**265,000/=**

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

A. MALENGO YA SHULE

Shule ya Sekondari KOM imelenga kumpatia kila mwanafunzi ufanisi wa hali ya juu kitaaluma na kijamii, kwa sababu hii tunasisitiza bidii katika kazi za kila siku na mazingira mazuri ya kujifunzia kwa lengo la kumwezesha mwanafunzi akue katika maadili mema. Kijamii, mwanafunzi atawezeshwa kujifunza katika vikundi, kuheshimu tofauti za kimaumbile na haki za binadamu, kutambua haki na wajibu wake katika jamii, mambo ambayo kila jamii inayahitaji katika ustawi wake.

B. NIDHAMU

Nidhamu ni sehemu muhimu sana katika Elimu. Nidhamu inapaswa kuwa sehemu ya maisha ya mwanafunzi kwani humjengea mwanafunzi kujitawala (kuwa na kiasi), kufuata taratibu za jamii, ufanisi na tabia njema.

Jambo la msingi katika nidhamu ya mwanafunzi ni kutilia mkazo masomo, kwaheshimu walimu, kujiheshimu yeye mwenyewe na kuwaheshimu wengine (wakubwa kwa wadogo)

C. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria, **Kanuni** na **Taratibu** za shule zinalenga katika:

- Kumwezesha mwanafunzi aweze kuishi katika mazingira ya amani, utulivu na mshikamano.
- Kumwezesha mwanafunzi aweze kutekeleza wajibu wake katika masomo na shughuli nyingine za kishule.
- Kumwandaa mwanafunzi kuwa raia mwema na mwadilifu katika nchi yake.
- Kumwezesha mwanafunzi awe na moyo wa kujituma na kujiamini.

Kwa hiyo ieleweke wazi kwamba sheria, kanuni na taratibu hizi za shule kulingana na malengo hayo hapo juu hazilengi katika kumkomoa au kumgandamiza mwanafunzi, bali kumjenga yeye binafsi pamoja na maisha yake ya baadaye.

Wanafunzi wanawajibika kuzifahamu sheria, kanuni na taratibu za shule, umuhimu wake na kuzifuata katika kipindi chote cha masomo. Sheria na kanuni zote za shule zitazingatiwa wakati wote mwanafunzi anapokuwa shuleni, nyumbani, kwenye usafiri wa shule na ziara zote za kishule.

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:

1. UYANYASAJI WA AINA YOYOTE ILE

Unyanyasaji kwa misingi ya utaifa, jinsia, dini, rangi, ulemavu, haiba kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, mwanafunzi na walimu au wafanyakazi shuleni hautaruhusiwa.

2. HESHIMA KWA WOTE

Wanafunzi wanapaswa kujiheshimu na kuwaheshimu walimu na watu wengine, wakubwa kwa wadogo. Mwanafunzi yeyote aposemeshwa na mwalimu, mfanyakazi wa shule au mgeni yeyote, anapaswa kusimama, kusalimia na kujitambulisha.

3. UVUTAJI WA SIGARA, KUBWIA MADAWA YA KULEVYA NA UNYWAJI WA POMBE YA AINA YOYOTE ILE.

Kwa misingi ya kisheria, kiafya, kitaaluma na kiusalama ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki au kutumia vitu vilivyoorodheshwa hapo juu.

4. UMILIKI WA SILAHA.

Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuja na silaha ya aina yoyote shuleni. Silaha hizi ni pamoja na; bunduki, bastola, kisu cha aina yoyote, rungu, au mfano wa silaha yoyote.

5. UTORO NA UZEMBE.

Utoro wa aina yoyote hauruhusiwi. Hii ni pamoja na:

(i) Kutohudhuria darasani, uzembe wa kutoshiriki kikamilifu katika shughuli zote za ndani na nje ya darasa.

(ii) Kutoroka shuleni wakati wa mchana au usiku aidha kwa kuruka uzio ama kupitia lango kuu pasipo ruhusa maalum.

(iii) Kutokufika au kuchelewa kufika shuleni siku ya kufungua shule (mwanafunzi ni lazima afike shuleni siku ya kufungua shule bila kukosa). Muda wa mwisho wa kufika shuleni ni saa 10.30 jioni, hii ni pamoja na kwa wale wote wanaopewa ruhusa fupi wawapo shuleni.

Wanafunzi wanapaswa kuwa na mahudhurio mazuri, kuwahi shuleni/darasani na kuomba ruhusa wanapokuwa na udhuru. Wanafunzi hawaruhusiwi kwenda likizo wakati wa muhula wa masomo.

6. UGOMVI, MATUSI NA KUPIGANA.

Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kupigana au kutumia lugha ya matusi au kuandika ujumbe wa matusi mahali popote akiwa shuleni au nje ya shule.

7. UTUNZAJI WA MAZINGIRA, MALI YA SHULE NA VITU VYAKE BINAFSI

Kila mwanafunzi atawajibika na utunzaji wa mazingira na usafi wa shule kwa ujumla. Wanafunzi wanapaswa kutunza na kulinda mali zote za shule kama vile majengo, meza, viti, vitanda, vitabu n.k. Pia mwanafunzi anapaswa kutunza na kulinda vitu vyake binafsi wakati wote. Mwanafunzi yeyote atakayebainika kuharibu vifaa na mali ya shule au ya wenzake atalipia gharama ya matengenezo au kununua kitu kipya. Mwanafunzi atalipia vitabu vya shule atakavyoviharibu au kupoteza.

8. CHAKULA

(i) UINGIZAJI WA CHAKULA SHULENI

Ni marufuku kwa mwanafunzi yoyote kuingiza au kuletewa chakula cha aina yoyote ile shuleni. Wanafunzi watakula chakula kinachoandaliwa shuleni tu.

(ii) ULAJI WA CHAKULA

Wanafunzi wote watakula chakula cha shule, ni marufuku mwanafunzi yeyote kutokula chakula kilichoandaliwa shuleni kwa sababu yoyote ile. Wanafunzi wenye matatizo ya kiafya yaliyothibitishwa na daktari wa serikali wataandaliwa mlo kulingana na matatizo yao.

(iii) USAFI NA NIDHAMU NDANI YA BWALO LA CHAKULA.

Wanafunzi watakula milo yao yote ndani ya bwalo. Ni marufuku kula chakula nje ya bwalo. Wakiwa ndani ya bwalo watakula kwa utaratibu mzuri na bila kupiga kelele. Wanafunzi watawajibika na usafi wa ndani na nje ya bwalo.

9. UTUNZAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI BINAFSI YA WANAFUNZI.

Pesa yote itakabidhiwa na kutunzwa na mhasibu wa shule. Kila mwanafunzi atafunguliwa akaunti yake. Hairuhusiwi mwanafunzi yeyote kukaa na kiasi chochote cha pesa bwenini au darasani.

10. MATUMIZI YA VITU VYA ELECTRONIKI NA UMEME.

Wanafunzi hawaruhusiwi kuja shuleni na vitu vya **electroniki na umeme** kama vile ***Pasi, Heater, Redio, Simu za mkononi, Redio kaseti*** na vitu vingine vya aina hii.

11. MAHUSIANO WA KIMAPENZI

Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kujihusisha na masuala ya mapenzi kwa namna yoyote ile, hii ikiwa ni pamoja na kuwa na picha zisizo na maadili, kuandika au kuandikiwa barua au maandishi yanayohusiana na mapenzi. Ni marufuku mwanafunzi kuonekana katika nyumba za kulala wageni, disko au baa hata wakati wa likizo anapokuwa nyumbani.

12. MATUMIZI YA KOMPYUTA, TV NA VIDEO ZA SHULE.

Wanafunzi watapaswa kutumia vifaa hivi kwa manufaa na uangalifu mkubwa sana, watavitumia vifaa hivi kwa idhini na usimamizi wa mwalimu husika. Wawapo darasani wasichezee video za kufundishia. Wanafunzi wanapokuwa katika maabara ya kompyuta wanapaswa kufungua tovuti zenye manufaa kitaaluma tu. Ufunguaji wa tovuti zisizo na maadili ni kosa. Aidha wanafunzi watafuata sheria na kanuni zote za maabara za sayansi na za kompyuta kama zitakavyokuwa zimeelekeza.

13. KINGA YA MOTO

Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha moto wa aina yoyote ile, isipokuwa kwa idhini maalum. Vifaa vya kuzima moto vimewekwa maeneo mbalimbali kwa tahadhari. Ni kosa baya sana kuchezea vifaa hivi au kubonyeza vifaa vya kutoa tahadhari ya majanga ya moto. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuwa na vianzisha moto kama vile viberiti, baruti au vitu vyenye kulipuka. Mwanafunzi atakayesababisha ajali ya moto, yeye pamoja na wazazi wake watagharimia gharama za kuuzima na fidia ya mali iliyoharibika.

14. TAHADHARI YA BARAZA LA SHULE.

Kila mwanafunzi atapaswa kuhudhuria baraza la shule na paredi zote kwa mujibu wa ratiba ya shule. Wakati huu atakaa kimya na kupokea maelekezo toka kwa viongozi wake na walimu.

15. SARE YA SHULE NA USAFI WA MWANAFUNZI

Uvaaji wa sare ya shule ni ishara na utambulisho wa kila mwanafunzi wa **Shule ya Sekondari KOM**. Hii ni sehemu ya nidhamu ya mwanafunzi shuleni. Sare hii itavaliwa na mwanafunzi muda wote awapo shuleni na katika shughuli zote za kishule.

Wanafunzi wote watalazimika kuwa na nywele fupi zilizonyolewa kwa mtindo wa kawaida. Uvaaji wa mapambo kama heleni, bangili, shanga, mikufu, hauruhusiwi. Ni marufuku kwa mwanafunzi kupaka rangi za kucha/midomo, wanja, kunyoa nyusi, kufunga kitambaa kichwani au kuvaa kofia akiwa katika sare ya shule.

Wanafunzi hawaruhusiwi kuvaa ndala au viatu vya wazi wakiwa wamevaa sare ya shule; watavaa viatu vya kawaida vya ngozi rangi nyeusi visivyo na kisigino kirefu (soli isiyozidi inchi moja).

16. MWANAFUNZI AKIWA DARASANI

Kwa kipindi chote mwanafunzi awapo darasani anapaswa kuwa na nidhamu na utii wa hali ya juu. Mwanafunzi haruhusiwi kuleta usumbufu wa aina yoyote kwa wenzake darasani kama vile kupiga kelele, kuzunguka ovyo darasani hata wakati wa vipindi vya kujisomea wenyewe.

17. MAMBO MENGINE YASIYORUHUSIWA SHULENI.

- Kusema uongo, kudanganya, kutazamia au kunakili zoezi au mtihani toka daftarini au kwa mwanafunzi mwingine.
- Kuuza kitu chochote shuleni.
- Kucheza kamari yoyote shuleni au mahali pengine popote.
- Kutafuna pipi, jojo, na mibuyu akiwa shuleni.
- Kujihusisha na mambo yoyote haramu.

18. UVUNJAJI WA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE NA MADHARA YAKE.

Sheria na kanuni za shule zilizoorodheshwa hapo juu zimegawanywa katika makundi matatu ya A, B na C; kulingana na uzito wa kila kosa. Hivyo kushindwa kutekeleza sheria na kanuni hizi kutapelekea mwanafuzi kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

KUNDI A:

- Uchelewaji
- Kutovaa sare sahihi ya shule
- Kutotunza nywele kama inavyopaswa.
- Kuweka rangi na dawa kwenye nywele, nyusi na kucha n.k
- Kutema mate ovyo na kutupa takataka ovyo.
- Kula chakula nje ya bwalo
- Kuleta na kutafuna jojo, pipi, mibuyu n.k
- Kutorudisha vyombo vya chakula mahali pake.
- Kuuza kitu chochote shuleni.
- Kunyofoa/kubandua matangazo kutoka katika mbao za matangazo bila pasipo idhini ya mwalimu.

KUNDI B:

- Kukwepa shughuli za shule kama vile usafi na shughuli zingine za nje.
- Utovu wa nidhamu darasani licha ya kuonywa.
- Kukaidi amri au maagizo halali ya viongozi wa wanafunzi.
- Matumizi ya lugha chafu, kashfa na matusi.
- Kuchezea vifaa vya kuzimia moto (fire extinguishers)
- Utoro wa aina yoyote mfano kutoka shuleni bila ruhusa maalum.
- Kushindwa kutimiza wajibu wako darasani/uzembe, Udanganyifu katika mitihani, mazoezi na majaribio au kughushi maksi na saini.
- Kugomea adhabu, kukaidi au kuonesha kiburi ama dharau kwa viranja, wafanyakazi wasio walimu, walimu au uongozi wa shule.
- Kupoteza au kuharibu kwa makusudi vifaa na mali nyingine za shule.
- Kujihusisha na masuala ya mapenzi mfano, kuwa kuwadi (kutumwa au kuagizwa masuala ya mapenzi), kuwa na picha za ngono, kuwa na barua au maandishi ya kimapenzi au kufungua tovuti za ngono.
- Kuanzisha moto pasipo idhini au kuonekana na vianzisha moto kama viberiti, baruti n.k.
- Kutokula chakula cha shule au kuleta chakula cha aina yoyote shuleni.
- Kuja na vifaa vya elektroniki na umeme shuleni kama vile simu za mkononi pasi, heater, redio n.k.
- Kukaa na kiasi chochote cha pesa bwenini au darasani.

KUNDI C:

- Uvunjaji wa mara kwa mara wa sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyo ainishwa katika kundi A na B.
- Wizi, udokozi, utapeli na kucheza kamari ya aina yoyote ile.
- Kujeruhi, kupigana, kutishia, kuonea au kunyanyasa wanafunzi wengine.
- Kuwa na sigara, tumbaku, mihadarati, madawa ya kulevya au vileo.
- Kutenda makosa ya jinai ndani au nje ya shule.
- Kupata mimba (wasichana) au kumpa mimba msichana (wavulana) shuleni ama nje ya shule.
- Kuchochea vurugu au kuwashawishi wanafunzi wengine kufanya makosa au migomo.
- Kutoroka shuleni kwa kuruka uzio wa shule au kupitia lango kuu bila kuwa na ruhusa iliyoidhinishwa.

AINA YA ADHABU

Adhabu zitatolewa kulingana na kundi la kosa alilolitenda mwanafunzi.

KUNDI A:

Makosa ya **kundi A** yatapewa adhabu zifuatazo:

- Karipio na onyo.
- Kuandika barua ya kuomba msamaha na kuahidi kutorudia tena kosa.
- Wakosaji wazoefu (wanaorudiarudia makosa) watapewa adhabu ya kazi nje ya darasa, au adhabu yoyote ile, ambayo itaonekana inafaa.

KUNDI B:

Makosa ya **kundi B** yatapewa adhabu kama ya kundi A, lakini kali zaidi, hii ni pamoja na:

- Kusimamishwa shule na kuwaleta wazazi shuleni ili wasaidiane na uongozi wa shule katika kurekebisha tabia ya mwanafunzi husika.
- Kuchapwa viboko mbele ya wanafunzi wote.
- Kuwaleta wazazi/walezi shuleni.
- Kufidia mali aliyoiharibu au kupoteza.
- Hatua au adhabu nyingine yoyote kadri uongozi wa shule utakavyoona inafaa.
- Kupewa adhabu ya kufanya kazi za nje.

KUNDI C:

Makosa ya **kundi C** yanaweza kupewa adhabu zifuatazo:

- Kusimamishwa shule na kuwaleta wazazi shuleni.
- Kuchapwa viboko mbele ya wanafunzi wote.
- Kufukuzwa shule.
- Ama vyote kwa pamoja.

N.B

- Kwa yale makosa ya jinai shule itashirikiana na vyombo vya dola.
  Maamuzi ya kumfukuza mwanafunzi shule yatapendekezwa na walimu na kuamuliwa na Bodi ya Shu

ii. <u>MAVAZI NA MAHITAJI MENGINE ANAVYOPASWA KUNUNUA MWANAFUNZI</u>

1. Viatu vyeusi vya ngozi Jozi mbili visivyo na kisigino kirefu na kiwi nyeusi ya kutosha.
2. Mikanda miwili ya ngozi - rangi nyeusi (kwa wavulana tu.)
3. Picha 4 za rangi za passport size.
4. Daftari kubwa (kurasa 160 au zaidi), mathematical set, penseli na kalamu za kutosha.
5. Begi dogo 1 jeusi kwa ajili ya kubebea daftari na vitabu.
6. Kufuli 2 ndogo kwa ajili ya kufungia dawati na sanduku lake.
7. Blanket 1 (rangi yeyote).
8. Pilo 1
9. Kanga pea moja kwa wasichana tu
10. Taulo
11. Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha.
12. Mafuta ya kujipaka ya kawaida yasiyo na manukato
13. Ndoo ndogo na beseni.
14. Nguo za michezo (Jozi mbili, rangi yoyote).
15. Raba za michezo jozi 1 na soksi za michezo jozi 2.
16. Kandambili – 1
17. Trak suti 1 isiyo fupi wala ya kubana
18. Nguo za kulalia (night dress 1)
19. Miswaki 2 na dawa ya meno ya kutosha robo muhula.
20. Sanduku dogo (Trunk) la kuenea vitu hivyo hapo juu tu.ina
21. Mfagio 1 wa kukaushia maji (squeezer) na mfagio 1 mlaini wa ndani.
22. Jembe na mpini.
23. Rimu 1 ya karatasi (photocopy paper A4 size) aina ya "***Double A***"
24. Fedha kwa matumizi binafsi. (Kiasi kisichozidi Tshs. 50,000/=).

<u>UTARATIBU WA MALIPO</u>

Malipo yote yafanyike katika akaunti ya shule **Na. 01J10-587034-00** iliyopo katika **Benki ya CRDB** tawi la **Shinyanga**, ama katika **Tawi lolote** la **benki ya CRDB**. **Malipo ya pesa taslimu hayakubaliki..**!!